# LEARNING BY EAR 2012

## “Bado ningali mwanadamu – Riwaya inayoangazia matatizo wanayopata wauguaji wa maradhi ya akili barani Afrika”

## EPISODE 9: “Tubadili mienendo yetu”

**AUTHOR: Chrispin Mwakideu**

**EDITORS: Andrea Schmidt, Pendo Paul**

**PROOFREADER: Pendo Paul**

**List of characters by scene:**

**SCENE ONE: MALEMBA NA CHUMBA WATEMBELEA KIKUNDI CHA WARUNDIFU “AUTISM CLUB”**

- **Malemba (MKE, 35)**
- **Triza (MKE, 30)**
- **Chumba ( MUME, 16)**
- **SAUTI ZA WAATHIRIKA (VIJANA 3-4, JINSIA MCHANGANYIKO)**
- **MSIMULIZI**

**SCENE TWO: VALERIE NA IRENE WAKO KATIKA KLINIKI YA DKT. MAHIRO**

- **Valerie (MKE, 19)**
- **Irene (MKE, 19)**

- **Mahiro (MUME, 50)**
- **MAKAMU WA RAIS (MKE, 55)**
- **MSIMULIZI**

**SCENE THREE: KAPAKA ARUDI NYUMBANI NA HABARI NJEMA**

- **Kapaka (MUME, 25)**
- **Cheupe (MKE, 25)**

**UTANGULIZI:**

Hujambo na karibu katika kipindi chetu cha redio kinachotupa fursa ya **Kunoa bongo, ili tujenge maisha yetu**. Hiki ni kipindi cha tisa katika hadithi iitwayo, **“Bado ningali mwanadamu”**. Hadithi inayoangazia masaibu ya wanaougua maradhi ya akili barani Afrika. Katika kipindi kilichopita, Kalama alipanga mkesha wa maombi ili kuyafukuza mapepo na majini yanayomtesa mpwa wake Chumba. Walakin, Malemba, mamake Chumba, hakufurahishwa na jambo hili, hasa pale Chumba alipoanza kukakamazwa na sauti hizo za waumini hao. Kwengineko, Kapaka alimtembelea aliyekuwa bosi wake hapo awali bwana Patel kule dukani ili kumshawishi amrudishie kazi yake ya ukeshia. Mkutano wao haukuzaa matunda. Vilevile, Irene alimpeleka rafikiye Valerie kwa Dkt. Mahiro baada ya Valerie kumtembelea chuoni. Usibanduke katika kipindi hiki cha leo kwa jina**‘Tubadili mienendo yetu”.** Tunaanza na Malemba na mwanae Chumba walipotembelea kikundi cha wagonjwa warundifu baada ya mkesha wa maombi kuambulia patupu. Aliyewapokea ni Triza, aliyejitolea kusaidia wagonjwa hao.

**SCENE ONE: MALEMBA NA CHUMBA WAKIFIKA KATIKA KIKUNDI CHA “AUTISM CLUB”**

1. **ATMO: MIXED VOICES OF TEENAGERS WITH AUTISM**

2. **MALEMBA:** Unaona, Chumba, nilikuwa sijui. Nilifikiri uko peke yako, lakini tazama! Kumbe mko wengi wenye matatizo kama yako.

3. **TRIZA:** Karibuni, karibuni katika kikundi chetu. Naitwa Triza mimi nimejitolea kutoa huduma hapa.

4. **MALEMBA:** Shukrani, Triza. Huyu ni mwanangu Chumba. Kwani kikundi hiki kilibuniwa lini?

5. **TRIZA:** Kama uonavyo, kila kitu ni kipya hapa. Kikundi hiki hakijamaliza hata mwaka mmoja. Watu wengi hawajui la kufanya na watoto wao wenye athari hii, na iwavyo kila uchao watoto wengi wenye athari hizi wanazaliwa. Ndipo mfadhili mmoja, asiyetaka kujulikana, alitoa fedha za kuanzishwa utaratibu huu. Nasikia pia yeye ana mtoto mwenye kuathirika hivi hivi.

6. **MALEMBA:** Hmm… na hapa watoto hasa wanafanya nini? Hii ni kama shule ama?

7. **TRIZA:** Kuna mambo mengi humu ndani, lengo letu kuu

ni kuwasaidia kujenga utangamano na watu na kuwasaidia waishi maisha ya kawaida.

8. **MALEMBA:** Na mtawezaje kuyafikia malengo yenu? Nimejaribu niwezavyo kwa miaka 16 na Chumba bila kufaulu. Siri ya ufanisi wenu ni ipi?

9. **TRIZA:** Kwa kweli hakuna siri. Tunachojaribu kufanya ni kumhudumia kila mtoto kivyake, na zaidi kuwahusisha kuhusiana wao kwa wao na hata sisi.

10. **MALEMBA:** Na wanachukuliaje huu mpango wenu? Hasa hawa watoto? Wanapendelea kweli?

11. **TRIZA:** Jitazamie! **(calls out)** Sawa, sikilizeni kila mmoja… tuna wageni! Tuwakaribisheni, sote tuwakaribishe. Moja! mbili! Tatu!! Haya!

12. **SFX:** **APPLAUSE AND CLAPS FROM TEENS**

13. **MALEMBA:** **(almost in tears)** Chumba! Wanakupigia makofi. Wanakukaribisha wewe! Angalau hapa ni pahala watu wanakuchukulia kama mwanadamu, anayestahili.

14. **CHUMBA:** Mamaa... Mamaa…

15. **TRIZA:** Chumba... tafadhali, njoo nikujulishe kwa

wenzako.

16. **MSIMULIZI:** Mito ya machozi ya furaha ikitiririka machoni mwa Malemba anapomuona Triza akimuongoza Chumba kwenye chumba kilicho na watoto wenye maradhi sampuli yake. Hebu tumbishie Dkt. Mahiro hodi kwenye chumba chake cha utahini walipo Valerie na Irene wameketi, wakisubiri kwa hamu atakalonena daktari baada ya Irene kumueleza yote yaliyotokea awali. Endelea kutega sikio.

**SCENE TWO: VALERIE NA IRENE KATIKA CHUMBA CHA UTAFITI CHA DKT. MAHIRO**

17. **ATMO: AT DR. MAHIRO’S EXAMINATION ROOM**

18. **MAHIRO:** Valerie, hali yako inahitaji matibabu endelezi tena ya haraka. Kwa hivyo, napendekeza uende kwenye hospitali za watu wenye matatizo ya akili.

19. **IRENE:** **(objecting)** Ati!? Hapana! Valerie hawezi kwenda huko. Hajaathirika sana, kama ni kunijua, pia anajijua. Isipokuwa hizo sauti tu hana shida nyingine. Kama utazizuia hizo sauti zisimfikie basi atakuwa amepona.

20. **MAHIRO:** Sikiliza, Bi. mdogo, nimefanya kazi ya udaktari kwa miaka mingi, na nimeona mengi. Kwa hivyo, nikisema apelekwe hospitali ya wenye maradhi ya akili, ujue ninafahamu nasema nini. Hii ni kwa ajili ya usalama wake mwenyewe, na akionyesha

dalili za kupona atatolewa.

21. **VALERIE:** Naruhusiwa kusema kitu?

22. **MAHIRO:** Bila shaka, wewe ndiye mgonjwa na una haki ya kusema unachotaka kuhusiana na hayo matibabu.

23. **VALERIE:** Nahitaji kwenda kwenye hiyo hospitali, iwapo itanipa ahueni… nataka kwenda.

24. **IRENE:** Lakini, Val! Unajua hadithi zote tunazozisikia kuhusu manesi wanaowapa dawa nyingi wagonjwa wa akili, ili waduwae na kutosema lolote. Unataka uwe hivyo?

25. **MAHIRO:** **(concerned)** Sasa, usimtishe mgonjwa wetu na hadithi hizo za kuogofya. Humhurumii? Najua watu wengi hawaziamini hospitali za akili, lakini niamini: yote tunafanya ili kusaidia wagonjwa. Madawa hayo ya akili athari yake inachukuwa muda mrefu, lakini hazidhuru mtu. Tuwaaminini wale wanaotuhudumia wagonjwa wetu. Hivyo tu ndiyo tutazipa hadhi hospitali zile kama nyenginezo.

26. **VALERIE:** Nahitaji kupona, nataka kurudia maisha yangu ya kawaida, masomo na…

27. **SFX:** **DOOR BEING KNOCKED DESPERATELY**

28. **MAHIRO:** Subiri wakati wako! Sijamaliza na hawa.

29. **SFX:** **DOOR BEING KNOCKED AGAIN**

30. **MAHIRO:** **(furious)** Ah, watu wengine hawaelewi lugha au ni nini. **(shouting)** Ngojeni kidogo…

31. **SFX:** **DOOR OPENED**

32. **M.R:** Wewe ndiye Daktari Mahiro?

33. **MAHIRO:** **(utterly confused)** Mheshimiwa… Sikujua ni wewe. Tukusaideje? Tafadhali karibia… karibu.

34. **IRENE:** Samahani, lakini wewe siye Makamu wa Rais?

35. **M.R:** Ni mimi, ndiye. Lakini niko kwa mambo yangu binafsi, kwa hivyo msiambie wengi kuja kwangu hapa. Singelipenda yeyote, hasa watangazaji habari kujua huwa naja kumuona mtaalamu wa akili.

36. **MAHIRO:** Kweli, wasichana, tupisheni kidogo. Mfikirie yale tuliyoambiana. Valerie anahitaji kwenda hospitali ya matatizo ya akili, na haraka itakuwa bora zaidi. Mimi mwenyewe nitachukuwa jukumu la kumhudumia akiwa

kule. Kwa hivyo msihofu. Atapona tu. Asanteni na karibuni.

37. **SFX:** **DOOR CLOSED**

38. **M.R:** Nashukuru kukubali kuniona kwa ghafla. Nafahamu ndiwe daktari pekee nchini na una kazi nyingi…

39. **MAHIRO:** Ndio ni kweli. Nimejaribu kuisukuma serikali iajiri wataalamu wengine lakini wapi. Lakini sidhani kama uko hapa kwa ajili ya masuala hayo?

40. **M.R:** Bila shaka. Najua hali ilivyo, niko hapo kwa ajili ya kijana wangu. Amezidiwa na sijui tena la kufanya.

41. **MAHIRO:** Oh, pole tutaona. Itanibidi nikamuone. Tunaweza kwenda huko sasa hivi tukiandamana.

42. **M.R:** Nilifikiri anapata nafuu, ameacha pia kule kubwabwaja. Lakini ghafla, amerudia ile hali yake ya kwanza kabla tuje tukuone.

43. **MAHIRO:** Kutibu maradhi ya urundifu kwa vijana si rahisi, na huchukua muda mrefu…

44. **M.R:** **(interrupts)** Sawa, hayo ushanieleza kitambo. Nitakacho ni msaada na kuniwekea siri.

45. **MAHIRO:** Nina wazo zuri zaidi: kwanini usiieleze hadhira?

46. **M.R :** **(shocked)** Ati nini? Kwani umerukwa na akili pia wewe? Nafikiri wewe huku kuuguza wenda wazimu kumekufanya pia wewe uwe wazimu?

47. **MAHIRO:** Watu wanahitaji kuona haya. Wajue kuwa maradhi haya yanashika mtu yeyote, hata kwa jamii ya wale wanaoongoza nchi.

48. **M.R:** La! Siwezi kufanya hivyo. Kwanza, wapinzani wangu wa kisiasa watapata nguvu za kunipiga vita, na pili, kijana wangu na familia yangu hawafai kupitia haya. Nimepoteza muda wangu bure kumleta hapa. Itabidi nimpeleke ng’ambo kwa matibabu.

49. **MAHIRO:** Sote tunahitaji kubadilisha mienendo yetu, mheshimiwa. Maradhi ya akili yanafaa kukubalika miongoni mwetu, kwenye jamii, na hata nchini. Hatuwezi kusema hatuyaoni. Watu wanateseka, kijana wako ni mmoja wa mamilioni ya watu wanaougu barani Afrika. Isitoshe, labda utakapojieleza hadhira itaweza kukuhurumia, au wengine wenye watoto na

maradhi kama ya kijana wako watakuunga mkono? Kama siasa ni wafuasi basi si hao? Na zaidi serikali inaweza kuweka uzito kwenye makadirio ya bajeti ya afya bora kwa wanaogua maradhi ya akili.

50. **M.R:** **(thoughtful)** Hmm… mbona sikufikira hivyo. Wote ulikuwa ni ubinafsi wangu. Kweli hakuna ajuae, labda hata naweza kuwa Rais kipindi kijacho. **(claps)** Sawa! Tufanye hivi! Utaendelea kumpa huduma. Usijali, pia nitakwenda kumshauri Rais atuongezee makadirio ya bajeti ya wizara ya afya.

51. **MSIMULIZI:** Dkt. Mahiro amefaulu kugeuza mawazo ya mtu muhimu sana katika uongozi wa nchi hii. Wakati daktari anapotoka kwenda kumuona kijana wa mheshimiwa, Kapaka alikuwa kizingitini kwake, amejaa furaha pomoni kwa yale yaliyotokea. Endelea kusikiliza.

**<u>SCENE THREE: KAPAKA AWASILI KWAKE NA HABARI NJEMA</u>**

52. **SFX:** **BUNCH OF KEYS FUMBLING.. DOOR OPENED**

53. **KAPAKA:** **(singing melodiously)**

54. **CHEUPE:** Kapaka! Tafadhali nyamaza, utamuamsha mtoto. **(shocked)** Mungu wangu siamini masikio yangu!

...Siamini!

55. **KAPAKA:** **(shocked too)** Kuna nini? Kumetokea nini? Uko sawa?

56. **CHEUPE:** Unaimba tena! Sikumbuki mwisho nilikusikia lini ukiimba. Ni tangu ufukuzwe kazi.

57. **KAPAKA:** **(proudly)** Basi, nimeajiriwa tena kazi. Kapaka amerudi kazini!

58. **CHEUPE:** **(almost in tears)** Mume wangu, nina furaha sana kwa ajili yako. Hii ni siku kubwa maishani mwangu. Hebu nieleze: umeajiriwa wapi?

**HITIMISHO:**

Tukitamatisha kipindi hiki cha tisa kwenye hadithi ile ya matatizo ya maradhi ya akili barani Afrika. Jiunge nasi kwenye kipindi cha kumi na cha mwisho kutathmini mwishoni mambo yatakuwaje. Je, Valerie atapata kupona? Vipi kumhusu Chumba? Na hivi Kapaka keshapata ajira, ndiyo maradhi yamemtoka?

Kwa hayo na zaidi usikose kipindi kijacho. Utakapo kusikiliza kipindi hiki au kingine kilichopita tembelea tovuti yetu www.dw.de/lbe. Waweza pia kutoa maoni yako katika ukurasa wetu wa facebook. Ni mpaka tutakapokutana tena. Kwa heri kwa sasa.